

MKATABA WA PANGO

KATI YA

ARYA MEDICAL CENTER LIMITED

NA

MODESTA J. WAMAHENGE

MKATABA WA PANGO

MKATABA HUU umefungwa leo tarehe 01 mwezi 06 mwaka 2025

KATI YA

ARYA MEDICAL CENTER LIMITED kampuni iliyosajiliwa Tanzania yenye S.L.P 13462 KINONDONI – DAR ES SALAAM (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “MPANGISHAJI”) kwa upande mmoja.

NA

MODESTA J. WAMAHENGE kampuni iliyosajiliwa Tanzania yenye S.L.P 10 KINODONI – DAR ES SALAAM (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “MPANGAJI”) kwa upande mwingine.

KWA KUWA:

- A. MPANGISHAJI ni Mmiliki halali wa Jengo la Kupangisha iliyopo Mtaa wa Kinondoni, kata ya Sinza C , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. Plot 1280 , Block 20 – Nyumba 21
- B. MPANGISHAJI bila kushawishiwa na mtu yeyote yule amekubali kumpangisha MPANGAJI nyumba hiyo tajwa hapo juu.
- C. MPANGAJI ameonesha nia ya kupanga eneo hilo kwa shughuli maalumu ya Biashara

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA haya yafuatayo:-

1. MPANGISHAJI amekubali mpangaji kupangisha nyumba hiyo kwa fedha za kitanzania shilingi Laki tano (500,000/=) kwa mwezi, fedha ambazo zitalipwa kila mwezi katika kipindi cha miaka mitatu **2025 - 2028**, ambapo ni sawa na fedha za kitanzania shilingi Milioni Sita (18,000,000/=).

2. Muda wa pango ni mwaka mmoja toka siku ama tarehe ya makubaliano baina ya pande zote mbili katika mkataba huu.
3. MPANGAJI atalipa fedha za kitanzania shilingi
500,000 kwa kila mwezi kwa muda wa miaka mitatu
kwa Mpangishaji, kupitia namba ya akaunti **01J1092793801** jina
MODESTA J. WAMAHENGE Benki **CRDB BANK** tarehe **01/06/2025**.
4. MPANGAJI atakuwa huru kutumia eneo hilo kipindi chote cha mkataba bila bugudha yoyote toka kwa MPANGISHAJI, na pia atawajibika kutunza mazingira ya eneo husika kwa usafi na usalama.
5. MPANGAJI atalipa kodi ya maji na umeme katika kipindi chote cha upangaji na huduma nyingine atakazokuwa anapata ambazo zinahitaji kulipiwa.
6. MPANGAJI atapaswa kutoa taarifa ya maandishi kwa kipindi cha miezi mitatu kabla kipindi cha mkataba kuisha kama atakuwa na nia ya kuendelea na mkataba.
7. MPANGAJI hataruhusiwa kupangisha eneo husika kwa Mtu mwingine au kwa jamaa yake bila idhini ya MPANGISHAJI. Pia mpangaji hataruhusiwa kubadili matumizi ya upangaji bila idhini ya MPANGISHAJI.
8. Endapo kutatokea mgogoro wowote katika mkataba huu, basi sheria husika za Tanzania zitatumika kutatua mgogoro huo.

KWA USHUHUDA HUU pande zote mbili zinaweka saini zao kushuhudia mkataba huu.

MKATABA HUU umewekwa SAINI na MUHURI hapa
DAR ES SALAAM Kny ARYA MEDICAL CENTER LIMITED

ARYA MEDICAL CENTER LIMITED
DAR ES SALAAM

MUHURI

leo tarehe 01/06/2025

Mwezi JUNE mwaka 2025

/

MBELE YETU:-

Jina Kamili : ENG. NAZIRU LUTHER KYARUZI

Sahihi : 

Anwani : P.O.BOX 13462 DAR ES SALAAM

Wadhifa : MANAGING DIRECTOR AT ARYA

Jina Kamili : MODESTA J. WAMAHENGE

Sahihi : 

Anwani : S.L.P 10 KINONDONI – DAR ES SALAAM

Wadhifa : Landlord – MWENYE NYUMBA

Witness to the above signature

Name CHUKLEDA PETER KLEBA MUKINDA

Signatures 

Postal Address P.O BOX 33520 DAR ES SALAAM

Qualification ADVOCATE

